

OFISI YA RAISI - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

MKUU WA SHULE
IPETA SEKONDARI
S.L.P 2337,
KILOLO
14/12/2021
SIMU - 0757-676663.

JINA LA MWANAFUNZI.....

S.L.P.....

KILOLO

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IPETA
WILAYA YA KILOLO MKOA WA IRINGA 2021**

1.0 UTANGULIZI.

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kijiunga na kidato cha **Kwanza IPETA SEKONDARI 2021**. Shule ipo umbali wa **KM. 45** kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **25/01/2021**

2.0. SARE ZA SHULE.

1. WAVULANA.

A. Suruali **2** za rangi ya **JANI LA MGOMBA**, mshono **CHINI UPANA 18 WENYE MKUNJO, YENYE MARINDA MAWILI, JUU YA MIFUKO YA MBELE NA MFUKO WA NYUMA USIWE NA ZIPU**. Mkanda wa suruali upana inch **2** wenge luksi (**NB. ZINGATIA RANGI YA KITAMBAA KILICOAMBATANISHWA NA FOMU HII**)

B. Mashati **2** meupe (tetron) mikono **MIREFU**.

C. Viatu jozi **2 vyeusi** vya kamba visivyo na kisigino kirefu.

- D. Soksi **jozi 4**. Au zaidi za rangi **nyeusi**
- E. Sweta **2. RANGI YA JANI LA MGOMBA yenyе V.** upande wa mbele isiyo na maandishi au mchoro wowote.
- F. Mkanda **mweusi** usiwe na nembo au mchoro au maandishi yoyote.
- G. Sare za michezo: Bukta **2 na** fulana **2 raba 1** na trakisuti ya rangi **NYEUSI**.

B. WASICHANA.

- A. Sketi **2** ndefu zinazovuka magoti rangi **JANI LA MGOMBA, Mshono: marinda 8. Ya kupanga yenyе mfuko upande wa kushoto, mkanda inch 2 (ZINGATIA RANGI YA KITAMBAA KILICHOAMABTANISHWA KWENYE FOMU)**
- B. Shati **2 nyeupe (TETRONI) mikono MIREFU.**
- C. Blauzi **2 nyeupe** za kuvalia ndani ya shati
- D. **Viatu jozi 2 vyeusi** vya kamba visivyo na visigino virefu
- E. Sweta rangi ya **JANI LA MGOMBA yenyе V.** upande wa mbele lisilo na maandishi au mchoro wowote.
- F. Kwa msichana wa kiislamu atavaa **HIJABU NYEUPE.**
- G. Sare za michezo: Bukta 2. na fulana 2 raba na trakisuti 1. rangi **NYEUSI**

3.0. VIFAA VYAKUJIFUNZIA.

1. Daftari **11** kubwa **kaunta books kwaya 2.**
2. Kalamu **5 na penseli 3**
3. Mkebe 1 kwa ajili ya somo la Hisabati
4. Begi la kubebea madaftari begi liwe imara
5. Rula 1.
6. Fagio la chelewa 1, Ndoo ndogo 1 hivi vifaa ni kwa ajili ya usafi wake binafsi.

4.0 MAHITAJI YA AFYA.

1. **Matibabu:** Mwanafunzi awe na kadi ya **CHF** (kadi ya bima ya afya) kwa ajili ya matibabu yake binfsi, na ikumbukwe kwamba matibabu ya mwanafunzi ni jukumu la **MZAZI** shule haitawajibika kwa matibabu ya mwanafunzi **shule inatoa huduma ya kwanza tu.**

5.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheri na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu ambayo inadhamana ya Elimu Nchini na ofisi ya Raisi TAMISEMI yenyé jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

- a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii yote kwa ujumla.
- b. Mahudhurio mazuri shuleni na katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d. Kuwahi shuleni na kufanya shughuli za shule na majukumu mengine utakayopangiwa na walimu na uongozi wa shule yako.
- e. Kufahamu kwa usahihi mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni
- f. Kutunza usafi wa mwili wako binafsi, mavazi yako na mazingira yote ya shule
- g. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
- h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- i. Kutunza mali za shule na uma wakati wote

5.1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga

3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, na Kubeli
5. Kupigana au kupiga mtu yeyote nje au ndani ya shule
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya uma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito au kupata mimba
9. Kuowa au kuolewa
10. Kutoa mimba au kumpa mimba mwanafunzi mwenzako
11. Kugoma, Kuchochea na Kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au jamii/watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkononi au laini ya simu.

KARIBU IPETA SEKONDARI KWA ELIMU, NA NIDHAMU

SAINI.....

JOACHIM J. MLAY.

MKUU WA SHULE

SIMU 0757-676663.